# HALMASHAURI YA WILAYA MUHEZA

## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA WILAYA TAREHE 20/10/2021

**WALIOHUDHURIA:**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mhe.Erasto J. Mhina | Diwani Kata Tongwe | Mwenyekiti |
| 2. Mhe.Salimu J.Sechambo | Diwani Kata Zirai | Makamu M/Kiti |
| 3. Mhe.Fuad R.Kibaja | Diwani Kata Kilulu | Mjumbe |
| 4. Mhe. Shabani A. Achimwene | Diwani Kata ya Makole | Mjumbe |
| 5. Mhe.Jestina Mtangi | Diwani Kata Misozwe | Mjumbe |
| 6. Mhe. Mwanaisha Mudhihiri | Diwani V/Maalum Muheza | Mjumbe |
| 7. Mhe.Saidi Z.Mtunguja | Diwani Kata Misalai | Mjumbe |
| 8. Mhe.Shabani M.Chewaja | Diwani Kata Kisiwani | Mjumbe |
| 9. Mhe.Moses K.Siwa | Diwani Kata Genge | Mjumbe |
| 10. Mhe. Victoria F Mgimba | Diwani Kata Kwabada | Mjumbe |
| 11. Bw. Msumari I Msumari | Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) | Katibu |

**WASIOHUDHURIA:**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mhe. Hamisi Mwinjuma | Mbunge jimbo la Muheza – | Kwa taarifa. |

**WATAALAMU WALIOHUDHURIA:**

| | |
|---|---|
| 1. Bw. Godhelp N Ringo | Afisa Utumishi Wilaya |
| 2. Bw. Hoyange M. Mbwambo | Afisa Kilimo, Ushirika Wilaya |
| 3. Bi. Kiope S. Salum | Afisa Habari Wilaya |
| 4. Bi. Herieth S. Nyangasa | Mratibu wa kudhibiti UKIMWI Wilaya |
| 5. Bw. Johari Mtango | Afisa Mtendaji Mamlaka ya Mji |
| 6. Bi. Vije Ndwanga | Afisa Maendeleo ya Jamii Wilaya |
| 7. Bi. Johari Kaira | Kaimu Afisa Biashara Wilaya |
| 8. Bw. Edward Mgaya | Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi Wilaya |
| 9. Bi. Magdalena Kimaro | Mratibu wa TASAF Wilaya |
| 10. Bw. Cyprian Mselemu | Afisa Mazingira Wilaya |
| 11. Bw. Richard Msagati | Kaimu Afisa Elimu Sekondari Wilaya |
| 12. Bi. Zaina Mzindakaya | Mweka Hazina Wilaya |
| 13. Bw. Nelson Mwankina | Afisa Uchaguzi Wilaya |
| 14. Bi. Rehema Akida | Kaimu Afisa Mipango Wilaya |
| 15. Dr. Habi Mwasangala | Kaimu Mganga Mkuu Wilaya |
| 16. Bw. Thomas Mkwavi | Kaimu Afisa Ardhi Wilaya |
| 17. Be. Yusufu Jengela | Afisa Mapato Wilaya |
| 18. Bw.Mkumbo L.Ngoi | Kaimu Afisa Tehama Wilaya |
| 19. Bi. Desderia Haule | Katibu Tawala Wilaya |
| 20. Bi. Aisha Mhando | Mwanasheria wa Halmashauri Wilaya |
| 21. Bi. Alice Cheche | Kaimu Katibu TSD Wilaya |
| 22. Bi. Furaha Sarakikya | Afisa Manunuzi Wilaya |
| 23. Bi. Pili Maximilian | Afisa Elimu MsingiWilaya |
| 24. Bi. Vumilia Saimanga | Kaimu Mkaguzi wa ndani Wilaya |
| 25. Bw.Obadia Msemo | Kaimu Afisa Misitu Wilaya |

26. Eng. Ramadhani Mtinge — Kaimu Mhandisi Ujenzi Wilaya
27. Bw. Walter Kiure — Kaimu Mthibiti Ubora Shule Wilaya

**MWANDISHI**

1. Bw. Gerald S. Gweba
2. Bi. Zaituni A Said

**6/2021/2022/47:** **KUFUNGUA KIKAO.**

Mwenyekiti alifungua kikao saa 04.45 asubuhi.

**6/2021/2022/48:** **KUTHIBITISHA AJENDA**

Katibu aliwasilisha ajenda za kikao na wajumbe walizikubali kama ifuatavyo:-

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha ajenda za Kikao
3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha tarehe 23/09/2021 na 28/09/2021.
4. Utekelezaji wa yatokanayo na kikao cha tarehe 23/09/2021.
5. Taarifa ya mapato na matumizi ya Halmashauri mwezi Septemba, 2021.
6. Taarifa ya mapato ya Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF, ICHF, PAPO KWA PAPO, Bima ya Afya ya Taifa NHIF), mwezi Septemba, 2021.
7. Taarifa ya marejesho ya mikopo ya vikundi vya Wanawake, Vijana na Walemavu mwezi Septemba, 2021.
8. Taarifa ya utekelezaji miradi ya maendeleo robo ya kwanza Julai - Septemba, 2021
9. Rasimu ya mpango mkakati wa Halmashauri kwa mwaka 2021/2022 - 2025/2026.
10. Taarifa ya kamati ya ukaguzi robo ya kwanza Julai-Septemba, 2021
11. Taarifa ya manunuzi robo ya kwanza Julai - Septemba, 2021
12. Kuwasilisha maombi ya marekebisho ya vifungu vya matumizi katika bajeti ya mwaka 2021/2022 kiasi cha Tshs. **2,266,883,200**
    i. Taarifa ya mapokezi ya fedha kiasi cha **Tshs 746,883,200/=**
    ii. Mapendekezo ya matumizi ya fedha za UVIKO 19 kutoka ofisi ya Raisi TAMISEMI kiasi cha **Tshs. 1,520,000,000/=**
13. Taarifa ya ziara ya ukaguzi wa miradi iliyofanywa na kamati ya Fedha
14. Taarifa ya Mkurugenzi (Machinga)
15. Masuala ya kiutumishi
16. Kufunga Kikao

**6/2021/2022/49.** **KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 23/09/2021 NA KIKAO MAALUMU CHA 28/09/2021**

Muhtasari wa kikao cha tarehe 23/9/2021 na muhtasari wa kikao maalumu cha tarehe 28/09/2021 ilisomwa na wajumbe wote na baadae Mwenyekiti na Katibu waliweka saini kuthibitisha kuwa ni kumbukumbu halali ya kikao hicho.

**6/2021/2022/50.** **UTEKELEZAJI YATOKANAYO NA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO TAREHE 20/10/2021**

**(a) TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI YA HALMASHAURI YA WILAYA MWEZI MEI 2021.**

i. Halmashauri iharakishe ukamilishaji wa uandaaji wa mikataba ili wapangaji wa vibanda vya ujenzi wapate mikataba hiyo na kusaini na hatimae Halmashauri ipate mapato.

ii. Watendaji wa Kata wakumbushwe kwa barua juu ya kusimamia mapato katika maeneo yao hasa maeneo yenye mageti ambayo mzabuni hajaweka mkusanya ushuru na njia zote zinazotumika kupitisha mazao ili kudhibiti upotevu wa mapato.

iii. Kufikia mwezi Disemba, 2021 Halmashauri iwe imeandaa andiko mradi kama maelekezo kutoka kikao cha ALAT yalivyoelekeza kwa kila Halmashauri. Miradi mkakati ni korona na "Crashier" ya kokoto.

**(b) KIBANDA CHA BIASHARA BRAVO**

(i) Taarifa kuhusu mkataba mpya wa upangaji wa eneo hilo ufanyike, na taarifa itolewe kikao kijacho

**(c ) NYUMBA ZA HALMASHAURI CHATUUR**

(i) Halmashauri iendelee na majadiliano walipe Milioni 40 za malipo ya awali na baadae wamalizie milioni 35. Taarifa itolewe kikao kijacho.

**6/2021/2022/51.** **TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI YA HALMASHAURI YA WILAYA MWEZI SEPTEMBA, 2021**

Katibu aliwasilisha taarifa ya mapato na matumizi ya Halmashauri ya Wilaya kwa mwezi Septemba, 2021. Nakala ya taarifa hiyo waligawiwa wajumbe wote. Kwa muhtasari taarifa hiyo ni kama ifuatavyo:-

## 1. MAPATO.:

Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Halmashauri ya wilaya ya Muheza imekisia kukusanya jumla ya Sh **34,325,867,500.00** kutoka kwenye vyanzo vyake vyote vya mapato. Hadi mwezi Septemba, 2021 Halmashauri imekusanya mapato ya ndani, ruzuku, na miradi ya maendeleo ya jumla ya Sh **7,958,091,448** sawa na 23% ya makisio

| CHANZO CHA MAPATO | Makisio 2021/2022 | Jumla ya Mapato Julai-Augost, 2021 | Mapato Halisi Septemba, 2021 | Jumla ya Mapato Julai - Septemba 2021 | ASILIMIA % |
|---|---|---|---|---|---|
| Mapato ya Ndani | 2,130,000,000 | 489,589,779 | 219,820,777 | 709,410,556 | 33 |
| CHF(Afya ya Jamii) | 180,000,000 | 10,930,061 | 10,714,060 | 21,644,121 | 12 |
| Ada za sekondari | 119,400,000 | 63,127,667 | 4,627,000 | 67,754,667 | 57 |
| Ada ya usafi na Mazingira | 20,412,000 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ruzuku Mengineyo | 779,075,000 | 259,668,196 | 32,918,446 | 292,586,642 | 36 |
| Ruzuku Mishahara | 23,046,673,000 | 3,768,821,080 | 1,934,006,600 | 5,702,827,680 | 25 |
| Ruzuku miradi ya Maendeleo | 8,067,507,500 | 707,188,706 | 447,047,604.24 | 1,154,236,310 | 14 |
| | **34,343,067,500** | **5,299,325,491** | **2,649,134,487** | **7,948,459,976** | **23** |

2. **MATUMIZI:**

Hadi kufikia mwezi Septemba, 2021, Halmashauri ya wilaya ya Muheza imetumia jumla ya TSh. **6,262,455,971** sawa na 20% ya bajeti ya 2021/2022.

| CHANZO CHA MAPATO | MAKISIO 2020/2021 | MATUMIZI JULAI AGOSTI 2021 | MATUMIZI SEPTEMBA 2021 | MATUMIZI JULAI SEPTEMBA 2021 | ASILIMIA % |
|---|---|---|---|---|---|
| Mapato ya Ndani | 2,130,000,000 | 247,811,038 | 163,331,004 | 411,142,042 | 19% |
| CHF(Afya ya Jamii) | 180,000,000 | 0 | 24,798,636 | 24,798,636 | 14% |
| Ada za sekondari | 119,400,000 | 23,763,947 | 17,150,400 | 40,914,347 | 34% |
| Ada ya Usafi na Mazingira | 20,412,000 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ruzuku Mengineyo | 779,075,000 | 204,532,316 | 28,236,590 | 232,768,906 | 30% |
| Ruzuku Mishahara | 23,046,673,000 | 3,768,821,080 | 1,931,266,600 | 5,700,087,680 | 25% |
| Ruzuku miradi ya Maendeleo | 8,067,507,500 | 364,537,924 | 98,429,739 | 462,967,663 | 6% |
| **JUMLA** | **34,343,067,500** | **4,609,466,305** | **2,263,212,969** | **6,872,679,274** | 20% |

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kuipongeza, ushauri ufuatao ulitolewa kwa wataalamu ili kuongeza mapato kwa Halmashauri.

- Juhudi za ukusanyaji madeni ziendelee kufanyika ili kupunguza au kumaliza madeni hayo. Kasi ya ukusanyaji mapato iongezwe hasa katika vyanzo ambavyo vipo chini ya asilimia 25 iliyoelekezwa.
- Kampuni ya EUTCO wataalamu wafuatilie ili ilipe deni kwa Halmashauri kwa kuwa kampuni inaelekea kufa.
- Usimamizi zaidi uimarishwe katika ukusanyaji wa mapato yanayotokana na machungwa ili kuepuka upotevu wa mapato.
- Halmashauri iweke mkakati ili kuweza kukuza zao la mihogo.

Taarifa ya mapato na matumizi ya mwezi Septemba, 2021 ilikubaliwa na kuwa kumbukumbu halali ya kikao hicho.

**6/2021/2022/52. TAARIFA YA MAPATO YA MFUKO WA AFYA YA JAMII (CHF, ICHF, PAPO KWA PAPO, BIMA YA AFYA YA TAIFA NHIF) KWA MWEZI SEPTEMBA, 2021**

Katibu aliwasilisha taarifa ya mapato ya mfuko wa Afya ya Jamii (CHF, ICHF Papo kwa Papo, Bima ya Afya ya Taifa NHIF) kwa mwezi Septemba, 2021. Nakala ya taarifa hiyo waligawiwa wajumbe wote.

Kwa muhtasari taarifa hiyo ni kama ifuatavyo:-

Kwa kipindi cha mwezi Septemba, Jumla ya **Tshs. 5,903,560/=** zimekusanywa kutokana na michango ya papo kwa papo, Jumla ya Tshs **4,356,736/=** kama malipo ya ICHF ya mwezi Aprili-Julai Jumla ya Makusanyo yote ni **TShs 10,443,796/=**. Kwa kipindi cha mwezi Septemba, 2021 hatukupokea malipo ya NHIF (ICHF tunadai malipo ya Februari-Machi na Agosti-Septemba, NHIF Julai-Septemba)

Aidha tangu kuzinduliwa kwa CHF Iliyoboreshwa tarehe 10/10/2019 jumla ya kaya **1,928** zimejiunga sawa na asilimia **14.2** ya kaya lengwa **13,560** ifikapo Juni 2022.

Kwa kipindi cha Mwezi Septemba 2021 vituo vya kutolea huduma za Afya vimetoa huduma kwa makundi ya msamaha zenye thamani ya **Tsh.38,971,609/=** Gharama hizi zinahushisha misamaha ya watoto chini ya miaka 5, wajawazito na wazee. Na gharama hizi ni kuanzia kumuona daktari, vipimo na dawa.

**MIKAKATI YA KUFIKIA LENGO LA UANDIKISHAJI WA ICHF.**

1. Kufanya ufuatiliaji wa malipo ya ICHF kutoka Mkoani kwa ukaribu ili kuviwezesha vituo kupata fedha ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba.
2. Kusimimamia vituo vya kutoa huduma za afya kutoa huduma zinazostahiki kwa wateja wa ICHF.
3. Kusimamia matumizi ya dawa na vifaa tiba kwa vituo vya kutolea huduma za afya.
4. Kuendelea kufanya uhamashishaji wa ICHF kupitia mikutano ya hadhara, shule, vikundi vya ujasiriamali, Walegwa wa Tasaf na vikundi vya Boda Boda.
5. Kufanya usimamizi shirikikishi katika vituo vya kutolea huduma za Afya na maafisa wasajili kuangalia idadi ya fomu ambazo hazijaingizwa kwenye mfumo na ambazo hazisomi kwenye mfumo wanachama wa ICHF walioandikishwa laikini hawajaingizwa kwenye mfumo.

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kuijadili, ushauri ufuatao ulitolewa;

i. Halmashauri ijitahidi kuongeza madawa katika vitua vya afya ili kuboresha huduma za afya kwa wananchi, sambamba na hilo Halmashauri iendelee kutuma maombi ya kupatiwa watumishi hasa wa kada za afya ili kupunguza upungufu uliopo.

Taarifa ya Mapato ya Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF, ICHF, Papo kwa Papo, Bima ya Afya ya Taifa NHIF) kwa mwezi Septemba, 2021 ilipokelewa na kuwa kumbukumbu halali ya kikao hicho.

**6/2021/2022/53:** **TAARIFA YA MAREJESHO YA MIKOPO KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WALEMAVU MWEZI SEPTEMBA, 2021.**

Katibu aliwasilisha taarifa ya marejesho ya mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na walemavu kwa mwezi Septemba, 2021. Nakala ya taarifa hiyo waligawiwa wajumbe wote, kwa muhtasari taarifa NI kama ifuatavyo.

Kwa kipindi cha mwaka 2021/2022 Halmashauri imetenga Tshs 213,000,000/= kwa ajili ya kutoa mikopo kwa vikundi 42 vya uzalishaji mali vya wanawake, vijana na Watu wenye walemavu. Kwa kipindi cha robo ya kwanza (Julai- Septemba -2021) fedha za mikopo zenye thamani ya Tshs 86,000,000/= zinatarajiwa kutolewa kwa vikundi 11 (ambapo fedha za marejesho ni Tsh. 37,000,000/= na mapato ya ndani ni Tsh. 49,000,000/=) kwa mchanganuo ufuatao.-

- Vikundi 5 vya Wanawake Tshs. 36,800,000/=
- Vikundi 4 vya Vijana Tshs. 36,800,000/=
- Vikundi 2 vya Walemavu Tshs. 12,400,000/=

**MAREJESHO YA MIKOPO YA VIKUNDI KWA KIPINDI CHA MWEZI SEPTEMBA 2021 KWA VIKUNDI VYA MWAKA 2010-2021**

Kwa kipindi cha Septemba 2021 jumla ya Tshs. **20,310,200/=** zimerejeshwa kwa mchanganuo ufuatao : -

- **Kwa vikundi vilivyokopeshwa kwa mwaka wa fedha 2019-2020 na 2020/2021**

| | | |
|---|---|---|
| Vikundi vya wanawake | Tshs. | 9,961,000/= |
| Vikundi vya Vijana | Tshs. | 6,279,000/= |
| Vikudi vya Walemavu | Tshs. | 918,000/= |
| **JUMLA** | **Tshs.** | **17,158,000/=** |

Kiasi kilichotarajiwa kurejeshwa kwa kipindi cha mwezi Septemba ni **Tshs. 37,345,083/=** (Vikundi hivi vipo katika muda wa marejesho).

- **Kwa vikundi vilivyokopeshwa mkopo kwa mwaka wa fedha 2010 hadi 2018.**

| | | |
|---|---|---|
| Vikundi vya wanawake | Tshs. | 2,132,200/= |
| Vikundi vya Vijana | Tshs. | 1,020,000/= |
| Vikudi vya Walemavu | Tshs. | 0 |
| **JUMLA** | **Tshs.** | **3,152,200/=** |

Kilichotarajiwa kurejeshwa kwa mwezi Septemba ni Tsh.**133,750,650/=** Deni Tsh, **130,598,450/=** ( vikundi hivi vimepitisha muda wa marejesho).

**CHANGAMOTO**

- Vikundi vilivyokopeshwa kwa muda mrefu kuanzia mwaka 2010 hadi 2018 Kutokurejesha madeni ya mikopo pamoja na jitihada mbalimbali zilizofanyika.
- Kutokupatikana kwa vikundi vya Watu wenye Ulemavu kunasababisha uwiano wa utoaji wa mikopo kutokwenda sawa (4 /4 /2).

**MIKAKATI NA UFUMBUZI**

- Vikundi vyote vilivyopitisha muda mrefu wa marejesho taratibu za kuhakiki upya umeandaliwa na taarifa zimeanza kutolewa kwa viongozi ngazi ya kijiji na kata ili kuweza kubaini uhai wa vikundi hivi upya na kazi hii imeshaanza kwa baadhi ya Kata (Magila, Kilulu, Kwakifua, Pande darajani na Kwamkabala).
- Wananchi na viongozi ngazi zote kuhamasisha walemavu waliopo katika vijiji na kata husika ili waweze kunufaika na mikopo hii.

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kujadili, ushauri ufuatao ulitolewa;

i. Ufuatiliaji uendelee kufanyika ili kubaini vikundi ambavyo vimeshalipa na vinaendelea kuonekana ili kupunguza madeni yanayoonekana.

Taarifa ya marejesho ya mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na walemavu mwezi Septemba, 2021 ilipokelewa na kuwa kumbukumbu halali ya kikao hicho.

**6/2021/2022/53.** **TAARIFA YA UTEKELEZAJI MIRADI YA MAENDELEO ROBO YA KWANZA JULAI - SEPTEMBA 2021**

Katibu aliwasilisha taarifa ya utekelezaji miradi ya maendeleo robo ya kwanza Julai - Septemba 2021, nakala ya taarifa hiyo waligawiwa wajumbe wote na kwa muhtasari ni kama ifuatavyo:-

Kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 Halmashauri ya wilaya ya Muheza imekisia kutumia kiasi cha Shs. 9,377,538,539.00 kwa ajili ya miradi mbalimbali ya Maendeleo kati ya fedha hizo kiasi cha Shs 852,000,000.00 ni makisio ya miradi ya mapato ya ndani na Shs 8,067,507,500.00 ni makisio ya miradi ya maendeleo kwa fedha toka Serikali Kuu kwa mwaka 2021/2022 na Shs. 458,031,039 ni fedha zilizopokelewa nje ya bajeti ya mwaka 2021/2022. Hadi kufikia mwezi Septemba, 2021 kiasi cha Shs. 955,681,175.00 kimepokelewa, kati ya fedha hizo kiasi cha Shs 479,705,197.00 ndicho kilichotumika. Muhtasari wa Fedha za miradi rejea jedwali hapo chini:-

| S/N | MIRADI | MAKISIO 2021/2022 | JUMLA MAPOKEZI JULAI 2021-SEPTEMBA, 2021 | MATUMIZI JULAI 2021 MPAKA-SEPTEMBA 2021 | % MAPOKEZI | % MATUMIZI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Miradi Mapato ya ndani | 852,000,000 | 167,000,000 | 162,441,170 | 20 | 97 |
| 2 | Under 5 Birth Registration (U5BR) | 10,000,000 | - | - | - | - |
| 3 | TASAF | 1,400,435,000 | - | - | - | - |
| 4 | SEQUIP | 1,675,200,000 | - | - | - | - |
| 5 | Malaria | 2,827,000 | - | - | - | - |
| 6 | NTD | 15,549,000 | - | - | - | - |
| 7 | Kampeni ya kitaifa ya Usafi wa Mazingira | 24,000,000 | - | - | - | - |
| 8 | Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya | 800,000,000 | - | - | - | - |
| 9 | Ukamilishaji wa Zahanati | 150,000,000 | - | - | - | - |
| 10 | AMREF-HIV/AIDS Support Program -HIV/AIDS | 20,740,000 | - | - | - | - |
| 11 | TB Grants | 5,308,000 | - | - | - | - |
| 12 | Elimu bila Malipo shule za msingi | 709,965,000 | 97,667,419 | 97,667,419 | 14 | 100 |
| 13 | Elimu bila Malipo shule za Sekondari | 799,907,500 | 63,196,077 | 48,974,968 | 8 | 77 |
| 14 | Mitihani (Msingi na Sekondari) | 758,047,000 | 169,786,640 | 169,786,640 | 22 | 100 |
| 15 | Miundombinu ya Elimu (Maabara za sayansi) | 150,000,000 | - | - | - | - |
| 16 | Miundombi ya Elimu (Madarasa Elimu Msingi) | 112,500,000 | - | - | - | - |
| 17 | Miundombinu Elimu (Madarasa Elimu Sekondari) | 112,500,000 | - | - | - | - |
| 18 | EP4R | 693,163,000 | - | - | - | - |
| 19 | LANES | 168,580,000 | - | - | - | - |
| 20 | Mfuko wa Jimbo | 51,001,000 | - | - | - | - |
| 21 | Mfuko wa Afya (Basket Fund) | 407,785,000 | - | - | - | - |
| 22 | Ruzuku nje y Bajeti | 458,031,039 | 458,031,039 | 835,000 | 100 | 0 |
| | **JUMLA MIRADI** | **9,377,538,539** | **955,681,175** | **479,705,197** | **10** | **50** |

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo.

Taarifa ya utekelezaji miradi ya maendeleo robo ya kwanza Julai - Septemba, 2021 ilikubaliwa na kuwa kumbukumbu halali ya kikao hicho.

**6/2021/2022/55:** **RASIMU YA MPANGO MKAKATI WA HALMASHAURI KWA MWAKA 2021/2022 - 2025/2026**

Katibu aliwasilisha Rasimu ya mpango mkakati wa Halmashauri kwa mwaka 2021/2022 - 2025/2026, nakala ya taarifa hiyo waligawiwa wajumbe wote na kwa muhtasari taarifa ilikuwa kama ifuatavyo:-

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Mipaka ya Wilaya

Wilaya ya Muheza ipo kati ya latitude 4" 54' 18" Kusini na Longitude 38" 55' 23" Kaskazini mashariki mwa Mkoa wa Tanga. Wilaya ipo upande wa Magharibi na Kusini Mashariki mwa Jiji la Tanga, kwa upande wa Magharibi inapakana na Wilaya ya Handeni na Wilaya ya Korogwe, Upande wa Kusini inapakana na Wilaya ya Pangani na kwa Upande wa Kaskazini inapakana na Wilaya ya Mkinga.

#### 1.1.1 Mamlaka ya Mji Mdogo

Halmashauri ina Mamlaka ya Mji Mdogo wa Muheza iliyoanzishwa kupitia tangazo la Serikali N. 537 la tarehe 19/7/2019 na ina kata 6 za Masuguru, Mbaramo, Tanganyika, Kwemkabala, Majengo na Genge. Kikao cha Baraza la Madiwani kilipendekeza kuongeza kata 8 ambazo ni Kicheba, Lusanga, Ngomeni, Kigombe, Magila, Kilulu, Tingeni na Mpapayu. Katika kata 14 Mamlaka ina jumla ya watu 57,515 kwa mujibu wa takwimu za sensa ya mwaka 2012.

### 1.2 Maeneo ya Kiutawala

Wilaya ya Muheza ilianza mwaka 1974, ambapo ilimegwa kutoka Wilaya ya Tanga. Wilaya ina Jimbo 1 la Uchaguzi, Tarafa 4, Kata 37, vijiji 126 na Vitongoji 494 na Mamlaka ya Mji Mdogo wa Muheza. Makao Makuu ya Wilaya ya Muheza yapo katika Mji wa Muheza ambao upo umbali wa kilometa 34 kutoka Jiji la Tanga. Ukubwa wa Wilaya ni Kilometa za mraba 1,974.

**Jedwali Na. 1: Idadi ya Kata, Vijiji na Vitongoji**

| JINA LA TARAFA | IDADI YA KATA | IDADI YA VIJIJI | IDADI YA VITONGOJI |
|---|---|---|---|
| Amani | 6 | 24 | 88 |
| Bwembwera | 8 | 35 | 149 |
| Ngomeni | 9 | 32 | 119 |
| Muheza | 14 | 35 | 166 |
| **JUMLA** | **37** | **126** | **494** |

**SURA YA PILI**

## 1.0 HALI YA SASA NA UTENDAJI

### 1.1 Mamlaka na Ngazi za Serikali za Mitaa

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 chini ya kifungu cha 6, ibara ya 145 na 146, na sheria zingine ndogo zinazohusiana, pamoja na; Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287 ya mwaka 2002; Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288 iliyorekebishwa mwaka 2002 na Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290 iliyorekebishwa mwaka 2002, inazipa mamlaka Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) nchini Tanzania jukumu la kufanya kazi kama vile; Utunzaji wa sheria, utaratibu na utawala bora; Kukuza ustawi wa kiuchumi na kijamii ndani ya eneo lake la Mamlaka; Utoaji wa huduma sahihi na kwa usawa kwa wananchi wa maeneo yao ya mamlaka, ukusanyaji sahihi na matumizi ya mapato ya Halmashauri pamoja na haki na kuwa na nguvu ya kushiriki na kushirikisha wadau katika kupanga na kutekeleza mipango/ programu za maendeleo.

Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ni moja kati ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa 185 nchini Tanzania, iliyoanzishwa chini ya Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287 iliyorekebishwa mwaka 2002 ambayo ililenga kuimarisha na kukuza mfumo wa Serikali za mitaa kuwezesha ushiriki wa jamii katika utawala wa ndani na usimamizi wa huduma za kijamii na kiuchumi katika maeneo yao ya mamlaka.

Majukumu ya Halmashauri ya wilaya kwa mujibu wa sheri za uanzishaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ni pamoja na:-

i. Kuwezesha na kudumisha amani, utulivu na utawala bora ndani ya eneo lake la Mamlaka
ii. Kukuza ustawi wa jamii na ustawi wa uchumi wa watu wote katika eneo ndani ya Mamlaka yake.
iii. Kwa kuzingatia sera ya kitaifa na Mipango ya Maendeleo Vijijini na Mijini, ili kuendeleza maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya eneo lake la Mamlaka

**Muundo.**

Katika Mpango mkakati uliopita muda wake Halmashauri ilikuwa na idara 16 ambavyo na Kilimo Umwagiliaji na Ushirika, Mifugo na Uvuvi, Ardhi na Maliasili, Maendeleo ya Jamii, Mazingira na taka ngumu, Afya na Ustawi wa Jamii, Fedha na Biashara, Utawala na Raslimali watu, Mipango takwimu na ufuatiliaji, Elimu Msingi, Elimu sekondari, Maji na Ujenzi na kulikuwa na vitengo 6 ambavyo ni Ukaguzi wa ndani, Uchaguzi, Manunuzi, Ufugaji nyuki, Sheria na Tehama. Mpango mkakati mpya unahusisha idara 15 na vitengo 6 kwakuwa idara ya maji haiko

katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na wamekuwa wakala wa Serikali kwa jina la RUWASA.

## 2.3 Mapitio ya Kiutendaji

Mapitio ya kiutendaji yamefanywa kwa kuzingatia malengo ya Mpango mkakati uliopita wa mwaka 2016/17- 2020/21. Changamoto zilizojitokeza zilibainishwa na kutatuliwa kwa ajili ya kuboresha utelekezaji wa Mpango mpya.

## SURA YA TATU: UCHAMBUZI WA HALI HALISI

### Scanisho ya Mazingira

Kama ilivyo kwa Mamlaka nyingine za Serikali za Mitaa nchini Tanzania, Halmashauri ya Wilaya ya Muheza inawajibika kutoa huduma kwa watu katika maeneo yake ya kimamlaka. Mafanikio ya utendaji huu yanategemea upatikanaji wa rasilimali watu pamoja na raslimali fedha

UUFC (SWOT) ni uchambuzi wa Taasisi kwa kuzingatia uwezo, udhaifu, fursa na changamoto. (i.e. tathmini ya raslimali) kwa kuzingatia fursa zilizopo na changamoto (tathmini ya mazingira).

### Uchambuzi wa mazingira ya ndani (Internal environmental analysis)

Sehemu ya ndani ya scanisho ya mazingira inahusu tathmini ya ndani ya Nguvu na Udhaifu wa Taasisi ambayo ni pamoja na kutathmini muundo wa sasa wa Halmashauri pamoja na utendaji wake.

### Uchambuzi wa UUFC (SWOC Analysis)

Mchakato wa uandaaji wa Mpango mkakati chini ya uchambuzi wa UUFC tumefanya mapitio ya scanisho ya Taasisi ya Halmashauri ya wilaya ya Muheza ili kupata taarifa ya mipango inayofaa kuhusu hali ya kimkakati ya ndani na nje ya mazingira. Hii itawezesha Halmashauri kuibua vipaumbele na mambo muhimu ya kuyashughulikia katika Mpango wa sasa na wa baadae.

Halmashauri kwa kupitia mchakato wa ushirikishwaji wa Wadau iliweza kuibua uwezo, udhaifu, fursa na changamoto.

## 3.3 Uchambuzi wa Wadau

Uchambuzi wa wadau ulimenywa kwa kushirikisha wadau mbali mbali wa Halmashauri ay wialaya ya Muheza. Uchambuzi huo uligundua na kutambua wadau, huduma inayotolewa na Halmashauri kwa wadau, matarajio ya wadau na athari zinayoweza kutokea (Endapo matarajio hayakufikiwa). Matokeo ya uchambuzi wa Wadau yameoneshwa kwenye jedwali hapo chini.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuijadili.

Rasimu ya Mpango Mkakati wa Halmashauri kwa mwaka 2021/2022 - 2025/2026 ilipokelewa na kuwa kumbukumbu halali ya kikao hicho.

**6/2021/2022/56:** **TAARIFA YA KAMATI YA UKAGUZI ROBO YA KWANZA JULAI - SEPTEMBA 2021**

Katibu aliwasilisha taarifa ya kamati ya ukaguzi robo ya kwanza Julai - Septembu 2021, nakala ya taarifa hiyo waligawiwa wajumbe wote na kwa muhtasari taarifa iyo ni kama ifuatavyo.

Katika kipindi cha Robo ya kwanza Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kimefanya ukaguzi katika maeneo mbalimbali ikiwemo Fedha na Biashara (Mapato na matumizi), Utumishi na Utawala, Manunuzi, TASAF III, Elimu Msingi na Sekondari, Kilimo na Umwagiliaji, Maendeleo ya Jamii, Afya,Mifumo ya FFARS,MUSE,LGRCIS na GOTHOMIS, na Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyopita ya Mkaguzi wa Ndani na Mkaguzi wa Nje.
Katika kipindi cha Robo ya kwanza (Julai – Septemba, 2021), Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kimefanya mapitio ya majibu ya hoja 21 za vipindi vilivyopita, hoja 15 zimefungwa na kubakia na hoja 6 zinazosubiri utekelezaji katika robo ya pili kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Pia katika kipindi cha robo ya kwanza, Julai hadi Septemba,2021 kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Mkaguzi ametoa hoja 12 ambazo bado zinaendelea kufanyiwa utekelezaji na Idara husika, hivyo kufanya kuwa na jumla ya hoja 18 zinazosubiri utekelezaji kutoka kwa Wataalamu.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuijadili.

Taarifa ya kamati ya ukaguzi robo ya kwanza julai - septemba 2021 ilipokelewa na kuwa kumbukumbu halali ya kikao hicho.

**6/2021/2022/57:** **TAARIFA YA MANUNUZI ROBO YA KWANZA JULAI - SEPTEMBA, 2021**

Katibu aliwasilisha taarifa ya manunuzi robo ya kwanza julai - Septemba, 2021, nakala ya taarifa hiyo waligawiwa wajumbe wote na kwa muhtasari ni kama ifuatavyo:-

Halmashauri ya Wilaya ya Muheza imefanya manunuzi yenye thamani ya **Tsh 146,905,973** (Milioni mia arobaini na sita, laki tisa na tano mia tisa sabini na tatu tu) kwa kipindi cha robo ya kwanza mwezi July-Septemba kwa mchanganuo ufuatao.

| | |
|---|---|
| • Vifaa | 142,265,973/= |
| • Huduma zisizo za kitaamu | 4,640,000/= |
| • Huduma za kitaalamu | - |
| • Kazi | - |
| **JUMLA TSH.** | **146,905,973/=** |

Wajumbe waliipokea tarifa na kuijadili.

Taarifa ya manunuzi robo ya kwanza Julai - Septemba 2021 ilipokelewa na kuwa kumbukumbu halali ya kikao hicho.

**6/2021/2022/58: TAARIFA YA MAREKEBISHO YA VIFUNGU VYA MATUMIZI KATIKA BAJETI YA MWAKA 2021/2022 KIASI CHA Tshs. 2,266,883,200/=**

Katibu aliwasilisha mapendekezo ya marekebisho ya vifungu vya matumizi katika bajeti ya mwaka mwaka 2021/2022 kiasi cha tshs. 2,266,883,200/=. Nakala ya taarifa hiyo waligawiwa wajumbe wote na kwa muhtasari taarifa ilikuwa kama ifuatavyo.

Halmashauri imepokea fedha nje ya bajeti kutoka serikali kuu kwaajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule za msingi na sekondari. Pia tunatarajia kupokea fedha kwaajili ya ujenzi wa chumba cha ICU katika Hospitali ya Wilaya. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo.

| S/N | SEKTA | CHANZO CHA FEDHA | KIASI |
|---|---|---|---|
| 1 | AFYA | UFUATILIA CHANJO ZA UVIKO 19 | 57 ,566,061.14 |
| | | UVIKO 19 IMF | 100,000,000 |
| | | VITUO VYA AFYA | 250,000,000 |
| | | **JUMLA AFYA** | **407,566,061** |
| 2 | ELIMU MSINGI | UVIKO 19 IMF | 280,000,000 |
| | | EP4R | 189,944,759.7 |
| | | **JUMLA MSINGI** | **469,944,759.70** |
| 3 | ELIMU SEKONDARI | EP4R | 211,872,379.86 |
| | | UVIKO 19 IMF | 1,140,000,000 |
| | | MABOMA – MADARASA 3 | 37,500,000 |
| | | **JUMLA SEKONDARI** | **1,389,372,379.86** |
| | **JUMLA KUU** | | **2,266,883,200.56** |

Wajumbe waliipokea tarifa na kuijadili.

Taarifa ya marekebisho ya vifungu vya matumizi katika bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kiasi cha shilingi 2,266,883,200.56 ilikubaliwa na kuwa kumbukumbu halali ya kikao hicho. ( Mchanganuo umeambatanishwa)

Vikundi vya wajasiriamali vilivyopata mikopo kutoka Halmashauri. Nakala ya taarifa hiyo waligawiwa wajumbe wote na kuisoma.

Baada ya kuisoma wajumbe walitoa ushauri ufuatao kwa wataalamu;

i. Majengo ya shule hasa madarasa yaliyofikiwa hatua ya lenta Halmashauri ijitahidi kuweka utaratibu kwa kutenga fedha ili kuyamalizia kwani yanakaa` muda mrefu na mwisho yanaharibika.

ii. Katika bajeti inayokuja Halmashauri itenge fedha ya kukamilisha miundombinu ya shule kwa kuzingatia maeneo yenye uhitaji zaidi na yaliyoonyesha tayari jitihada.

- Taarifa ya ziara ya ukaguzi wa miradi robo ya kwanza Julai – Septemba, 2021/2022 ilikubaliwa na kuwa kumbukumbu halali ya kikao.

**6/2021/2022/60:** **TAARIFA YA MKURUGENZI (MACHINGA)**

Katibu aliwasilisha taarifa ya kuwapanga upya na kuwapatia nafasi wafanyabiashara wadogo mjini Muheza, nakala ya taarifa hiyo waligawiwa wajumbe wote na kuisoma. Kwa ufupi taarifa ilieleza kuwa, eneo la soko la samaki la zamani (MKUNGUNI) ni eneo rafiki salama na sahihi kwa wafanyabiashara wadogo kufanya biashara zao ili kulinda mitaji yao. Hii ni pamoja na kuweza kuwakutanisha na taasisi za kifeha kwaajili ya kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuijadili..

**AZIMIO**

Wafanyabiashara watakaa eneo hilo kwa muda wakati maandalizi ya kuwatafutia eneo lingine yanafanyika.

**6/2021/2022/61:** **MASUALA YA KIUTUMISHI**

Masuala ya kiutumishi yalijadiliwa.

**6/2021/2022/62:** **KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe na wataalamu kwa kufanikisha kikao. Alifunga kikao rasmi saa 8.20 mchana.

**UMETHIBITISHWA:**

.................................................
**KATIBU**

.................................................
**MWENYEKITI**

**TAREHE**...30/11/2021...